

HALMASHAURI YA WILAYA YA NKASI

MKOA WA RUKWA:

FAX: 025 283 0136

SIMU: 025 283 0006

Email: ded@nkasidc.go.tz

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb.Na.NKS/DC/M.30/I/VOL. I/80



Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W),
S. L. P. 2,
NAMANYERE - NKASI.

Tarehe: 03/04/2023

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI.

Halmashauri ya (W) ya Nkasi imepata kibali cha Ajira mpya mbadala toka Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma chenye **Kumb Na. FA.170/373/01" A"/51** cha tarehe **19.03.2023** ili kujaza nafasi hizo Mkurugenzi Mtendaji (W) ya Nkasi anakaribisha maombi kwa wataanzania wenye sifa kama ifuatavyo:-

1.0. Mtendaji wa Kijiji III (Nafasi 03)

1.1. Sifa za mwombaji:

Mwombaji awe amehitimu kidato cha nne (IV) au sita na mwenye cheti cha **Astahada** (NTA Level 5) kimoja wapo katika sifa zifuatazo:-

- Utawala
- Rasilimali watu
- Sheria
- Maendeleo ya Jamii
- Elimu ya Jamii
- Usimamizi wa Fedha au
- Sayansi ya Sanaa kutoka Chuo chochote kinachotambulika na Serikali.

1.2. Kazi na majukumu:

- Afisa masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji
- Kusimamia Ulinzi na Usalama wa Raia na mali zao, kuwa Mlinzi wa Amani na Msimamizi wa Utawala Bora katika Kijiji.
- Kuratibu na kusimamia upangaji wa utekelezaji wa mipango ya Maendeleo ya Kijiji
- Kuratibu Mikutano na kamati zote za Halmashauri ya Kijiji.
- Kutafsiri na kusimamia Sera, Sheria na taratibu za uendeshaji wa Serikali ya Kijiji.
- Kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasiha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umasikini na kuongeza uzalishaji mali.
- Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi Kumbukumbu zote na Nyaraka za Kijiji.

1.3. Mshahara.

- Atalipwa mshahara kwa viwango vilivyopo vya Serikali kulingana na cheo chake yaani TGS B1 - TGS B10.

2.0. DEREVA II (Nafasi 01)

2.1. Sifa za mwombaji:

Mwombaji awe amehitimu kidato cha nne (IV) au sita mwenye Leseni Daraja C ya uendeshaji pamoja na uzoefu wa kuendesha magari kwa muda usiopungua miaka mitatu bila kusababisha ajari. Aidha, awe amehitimu mafunzo ya ufundi na kuhitimu cheti toka VETA au chuo kingine kinachotambulika na Serikali.

2.2. Kazi na majukumu

- Kuendesha magari ya Halmashauri
- Kuhakikisha kuwa gari na vyombo vyake vipo katika hali nzuri wakati wote, na kufanya uchunguzi wa gari kabla na baada ya safari ili kugundua ubovu unaohitaji matengenezo.
- Kufanya matengenezo madogomadogo katika gari
- Kutunza na kuandika daftari la safari (Log Book) kwa safari zote.
- Kuchunguza na kutoa ripoti ya ubovu wa magari.

2.3. Mshahara.

- Atalipwa mshahara kwa viwango vilivyopo vya serikali kulingana na cheo chake yaani TGS B1 - TGS B10.

MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI WOTE.

- Waombaji wote wawe Raia wa Tanzania wenye umri kati ya miaka 18-45.
- Maombi yote yaambatishwe na cheti cha kuzaliwa pamoja na nakala za vyeti vya shule na vya taaluma husika.
- Maombi yote yaambatishwe maelekezo binafsi (CV) za mwombaji husika yenye anwani na namba za simu pamoja na majina ya wadhamini watatu na namba zao za simu.
- Maombi yote yaambatishwe na picha moja ya **passportsize** iliyopigwa hivi karibuni.
- **Testimonials, provisional Results, statement of Results, Hati za matokeo ya kidato cha IV na VI (yaani form IV and VI Result slips) havitakubaliwa.**

- Hatua kali za kisheria na kiutawala zitachukuliwa kwa watakaoghushi vyeti katika maombi haya.
- Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe **25/04/2023** saa **8:00** mchana. Aidha, Halmashauri ambayo ni www.nkasidc.go.tz, secretariat ya Ajira na kwenye mbao za matangazo.
- Maombi yanaweza kuandikwa kwa lugha ya Kiswahili fasaha au Kiingereza fasaha na yatumwe kwa posta kwa anwani ifuatayo:-

Mkurugenzi Mtendaji (W),
S.L.P 02,
NAMANYERE - NKASI.



.....
LADISLAUS MZELELA

KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W)

NKASI.

**MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
NKASI**

NAKALA:

- Katibu Tawala (M),
S.L.P 128,
SUMBAWANGA.
- Katibu Tawala (W),
S.L.P 128,
SUMBAWANGA.
- Ofisi za WEOS zote,
Halmashauri ya Wilaya,
NKASI.